


Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE): Baadhi ya Hatua Unazoweza Kuchukua

Ikiwa mtoto wako anastahiki Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE), wilaya ya shule itapendekeza programu ambayo wanaamini itamsaidia mtoto wako. Sheria na kanuni za Massachusetts zinalinda haki yako ya kufanya chaguo tofauti. Shirikiana na shule yako ili kuongeza ufaulu wa mwanafunzi wako!

Hivi ndivyo unavyoweza kufanya!


Unaweza kuwasilisha ombi la kusajiliwa kwa mtoto wako katika mpango wa Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE) kutoka kwa programu zinazotolewa na wilaya.



Unaweza kuhudhuria makongamano au mikutano inayopatikana ili kujifunza zaidi kuhusu programu za Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE) zinazotolewa katika wilaya.



Pia unaweza kutembelea programu inayopendekezwa ili kuona ikiwa inafaa mtoto wako. Unaweza pia kuomba programu tofauti au mpya ya Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE).



Unaweza kuchagua kutomsajili mtoto wako katika Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE). Unaweza pia kumwondoa mtoto wako kwenye programu baada ya kuanza.



Jifunze zaidi kutoka kwa Baraza la Ushauri la Mzazi kwa Wanafunzi wa Kiingereza (English Learner Parent Advisory Council, ELPAC) la wilaya yako, kundi la familia zinazokutana pamoja ili kuzungumza kuhusu Elimu ya Mwanafunzi wa Kiingereza (English Learner Education, ELE).

Nyenzo hii iliundwa kwa ajili ya Idara ya Massachusetts ya Elimu ya Msingi na Sekondari na Kituo cha Ushirikiano cha Familia cha Jimbo Lote la Massachusetts, mpango wa Shirikisho la Watoto Wenye Mahitaji ya Pekee.

Je, una maswali? Wasiliana na shule yako: